## Kozi za Muda (Short Courses) na Kozi Maalumu (Tailored Training Program) Zinazofundishwa:

- Sanaa za kiafrika (uchezaji ngoma za asili, upigaji ngoma na utengenezaji ngoma, muziki wa kisasa na wa asili, uigizaji, kupiga picha jongefu, Uhariri picha pamoja na Kiswahili kwa wageni)
- Kozi hizi hutolewa kulingana na uhitaji wa mteja.

Sifa za Kujiunga

- Uwezo wa kusoma na kuandika

.





**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

Mkuu wa Chuo
Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo
(TaSUBa)
S.L.P 32,
Bagamoyo, Pwani.
Barabara ya Kaole

## Namba za Simu:


**+255 762 544 613**
**+255 784 394 933**
**+255 766 264 581**

**Barua pepe:**
**tasuba@michezo.go.tz**
**application@tasuba.ac.tz**

**Tovuti:**
**www.tasuba.ac.tz**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

# TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)






## Kwa mafunzo bora ya Sanaa na Utamaduni

www.tasuba.ac.tz

## UTANGULIZI

Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) ni wakala wa Serikali iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali, Kifungu cha 245 kupitia Tangazo la Serikali Na. 220 la mwaka 2007, ikiwa na malengo ya kukuza, kuhifadhi na kutunza sanaa na utamaduni wa Mtanzania ikiwa chini ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

TaSUBa ni zao la Chuo cha Sanaa Bagamoyo kilichoanzishwa mwaka 1981, na kufikia mwaka 2007 ndipo kilipobadilishwa na kuwa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo.

## DIRA

Kuwa kituo cha Sanaa na Utamaduni Afrika chenye ubora Uliotukuka

## DHIMA

Kuzalisha Wasanii, Viongozi wa sanaa na Wafanyakazi katika sekta ya Utamaduni, sambamba na kuzalisha



**TaSUBa** inatoa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Astashahada (Cheti) na Stashahada (Diploma) pamoja na kozi za muda mfupi (Short Courses). Sifa za kujiunga na Astashada na Stashahada ni kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

### Kozi za Muda Mrefu Zinazofundishwa:

**1. Sanaa za Maonyesho na Ufundi**

(Performing and Visua Art)

- Muziki: Nadharia ya muziki, uongozaji muziki, upigaji wa vyombo vya muziki vya kisasa na vya asili
- Ngoma: Uchezaji wa ngoma za asili na kisasa, na uchezaji wa muziki wa kisasa
- Tamthiliya: Uigizaji wa filamu, uongozaji filamu, uigizaji wa jukwaani na radioni, na uandishi wa miswaada ya filamu.
- Sanaa za Ufundi: Uchoraji, uchoraji wa kutumia rangi, ufinyanzi, usanifu michoro maandishi na picha na michoro
- Ufundi wa jukwaa: Ufundi wa sauti, ufundi wa mwanga, na utengenezaji wa maleba

**2. Picha Jongefu (Film and TV Production)**

- Uchukuaji wa Video (Video Shooting)
- Uhariri wa Video (Video Editing)
- Uongozaji wa Filamu (Film Directing)
- Uandishi Miswada ya Filamu (Script Writing)

3. Uzalishaji wa Muziki na Sauti (Music and Sound Production)

- Kurekodi Sauti (Sound Recording)
- Kurekodi Muziki (Music Recording)
- Uzalishaji wa Muziki (Music Production)
- Usimamizi wa Studio (Studio Management)

## SIFA ZA KUJIUNGA

**Astashahada (Cheti)**

Mwombaji anatakiwa awe na sifa ifuatayo;

- Awe amehitimu kidato cha Nne (FORM IV) na kupata ufaulu wa kuanzia "D" Nne (4).

**Stashahada (Diploma)**

Mwombaji anatakiwa awe na sifa moja wapo kati ya hizi zifuatazo;

- Awe amehitimu kidato cha Sita (FORM VI) na kupata ufaulu wa kuanzia Principal Pass Moja (1) na Subsidiary Moja (1).
- Awe amehitimu ngazi ya Astashahada (Cheti NTA Level 4) kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na NACTVET.
- Awe amehitimu kozi ya Ualimu Daraja la III A.



